THE DISTANT BOAT

Mwongozo was kuambatana na Sinema

FILAMU KUHUSU AFRIKA, UMISHENI, KANISA NA JUKUMU LETU KUWAFIKIA WALIOPOTEA

WWW.DISTANTBOAT.COM

Utangulizi

Kazi ya Mungu wakati huu katika Afrika, kupitia mashirika ya injili, haiwezi kusimamishwa. Hata hivyo, kanisa la kristo katika Afrika linakumbwa na changamoto ya ongezeko la Uislamu. Waislamu wanafanya kila juhudi kuigeuza Afrika ifuate dini na utamaduni wao. Makanisa mengi Afrika hawana habari kuwa Uislamu katika Afrika una nguvu tunayohitaji kukabiliana nayo. Wengine wanajua, lakini wanasubiri muinjilisti mzungu aje awahubirie Waislamu walio karibu nao. Wengine wamenyamaza kimya wakihofia madhara fulani iwapo watazungumza. Ni hadi lini kanisa katika Afrika litatia kimya wakati wasichana, vijana, wanawake, na wanaume wanendelea kunyakuliwa na vuguvugu la Kiislamu?

Utume ulionenwa katika Mathayo 8:18-20 unajumuisha Waislamu. Hadi wahubiri, viongozi wa Kikristo, na ndugu na dada wote wachukue jukumu la kuwanenea Waislamu kazi haijakamilika na kanisa katika Afrika linasalia kuwa hafifu na matatizo. Wakati umefika kanisa katika Afrika lichukue jukumu la kuwatuma wamishonari kwa marafiki zao Waislamu, majirani, na jamaa zao. Kama kanisa halitakumbana na changamoto la Uislamu sasa, miaka michache baadaye hakutakuweko na muda wa kuamka na kuhubiri injili. Kwa urahisi, Afrika itakuwa inatawaliwa na Uislamu.

Ni vipi twaweza kueneza injili kati ya Waislamu wakati huu tunakumbwa na vizuizi vingi? Kwa sababu tunajua kuna tofauti kubwa baina ya imani yetu na ile ya Kiislamu, tunahitaji kumuinua Yesu kwa ile hali kwamba tuwavute watu kwake bila ya kuwazuia kuona Ukweli.

Hadithi ya Mashua ya Mbali

Mashua ya Mbali inasimulia maisha ya Max, kijana wa mjini aliyefaulu kwa mengi: kazi nzuri, rafiki wa karibu, msichana anayetarajia kufunga ndoa naye. Akiwa katika hali ya hatari, Max anaokolewa na mvuvi aitwaye Yusufu ambaye ni Muislamu. Watu wake hawana kanisa na hakuna mkristo anayewahuburia. Baadaye, akiwa likizoni kutembelea jamii yake, Max anazungumza na mjomba wake kuhusu watu kutoka kijiji cha Yusufu, na hapo ndipo max alianza kujihisi kama Mungu anamtuma awe mishonari kwao.

Lakini safari hiyo ilikumbwa na vizuizi. Lazima Max akubali kupoteza kila kitu – maisha yake ya baadaye, heshima anayopewa, na hato pendo la roho yake – anapofuata mwito huo. Rafiki zake walimkejeli, shtuma kutoka kwa wakwe, na madharau kutoka kwa familia yake. Kanisa lake halijawahi kuwa na mishonari Mkenya, na mchungaji wake hajui ni wapi pa kuanzia. Kwake Max, familia yake, marafiki, na kanisa, ni safari ya uvumbuzi kuelewa maana ya kuwa na kumtuma mishonari, na sababu ya hiyo gharama.

Kuhusisha kanisa lako

Mashua ya Mbali inalenga kulichangamsha kanisa lako kutazama makundi mengi yaliyo karibu nanyi na hawajafikiwa na ujumbe wa injili ya Yesu Kristo. Filamu hii ni chombo cha kuwasisimua waumini warejee Uinjilisti. Kupitia kwa sanaa mwafaka na hadithi, filamu hii inawalenga wengi na ujumbe muhimu. Filamu hii inatarajiwa kudai majibu kutoka katika umri mbali mbali kutoka kwa vijana hadi watu wazima.

Mwongozo wa Mafunzo

Mwongozo huu unaambatana na filamu ya *Mashua ya Mbali*. Kusudi lake ni kuhakikisha kwamba baada ya filamu, watazamaji wanaweza kushughulikia mambo kadhaa muhimu yanayoangaziwa. Lengo ni kusisimua majibu ya kina kwa kila mmoja na kwa jumla kama kanisa.

Mawaidha kwa viongozi wa vikundi.

Unapoongoza kikundi chako – kama ni katika masomo ya jumapili au kikundi cha nyumbani, kamati ya umisheni, ama kundi lililokuja pamoja kwa kongamano – elewa ya kwamba unawaongoza kwenye njia ya uvumbuzi. Kuna mafunzo mengi kupitia kwa filamu hii ya *Mashua Ya Mbali*. Masomo sita yametengwa ili kusaidia mazungumzo kwa kuambatanishwa katika mwongozo huu.

Ni muhimu maswali yatumiwe kusisimua mazungumzo. Kama kiongozi wa mazungumzo, hakikisha wanenaji wanatoa maoni na mtazamo wao kwa wazi bila ya vikwazo. Jukumu lako ni kuuliza maswali, kuihimiza mazungumzo, na kusaidia watoe majibu yanayoambatana na lengo la filamu – na mwishowe, yanayokubaliana na Maandiko Matakatifu.

Kila somo linaangazia sehemu fulani ya filamu ambayo ni muhimu muitazame kwanza kabla ya mazungumzo. Sehemu hizo za filamu zipo katika kitengo cha “Mwongozo wa Mafunzo.” Kila somo limeandika vifaavyo. Masomo haya yanaweza kupatikana **www.distantboat.com**, bila malipo na kuchapishwa ili yatumiwe inavystahili.

Katika kila somo, maswali yanaambatana kwa mtindo sawa: maswali ya kutazama, kutafakari na kutenda.

Tunaamini wewe na kikundi chako mtafurahia safari hii ya uvumbuzi, na kwamba nyote mtaguswa na ukweli mtakaoupata

Somo la kwanza
Ni nani aliye kwenye Mashua ya Mbali?

"Usichekelee mashua iliyo mbali ikisombwa na mawimbi.
Labda ndugu yako yuko ndani."

Maswali ya Mazungumzo au Kutafakari

Tazama: *Methali ya Nzomo* 01:31:40–1:32:40; *Mahubiri mithali* 01:44:04–01:45:19

1. Unaelewaje msemo huu kutoka Afrika ulionakiliwa na Mjomba Nzomo?

2. Kulingana na mjomba Nzomo, katika msemo huu, ndugu yako ni nani?

3. Ni nani anachekelea mashua iliyo mbali?

4. Unadhani ni nini kitafanyika kama mashua itazidi "kuchekelewa"?

5. Je, ushawahi kutowazingatia wale hawajafikiwa? Kwa njia gani?

6. Ni kwa namna gani Kanisa, kwa jumla, halijazingatia wale hawajafikiwa?

7. Kwa nini sisi pamoja na makanisa yetu, tuwe na shughuli kuhusu makundi ya watu ambao hawajafikiwa?

Neno **"Hawajafikiwa"** lina maana gani?

"Wale hawajafikiwa ama kufikiwa kidogo ni kikundi cha jamii ambacho hakuna waumini Wakristo wakiasili walio na raslimali tosha kuwahubiria jamii kwa jumla."
www.joshuaproject.net



Mawazo ya Mwisho

Kama mchungaji Wambira alivyonena, "kwa kawaida sisi huwapenda walio wetu." Ingawa, ukweli ni kwamba katika makabila na makundi mengi ya watu hamna kanisa miongoni mwao. Hawajawahi kusikia injili ya Yesu Kristo! Na hawataisikia injili kama hatutaacha "kuwapenda wale wetu" na "kuipenda ulimwengu" mzima kama aipendavyo Mungu.

Ujumbe wa Aya ya Kumbukumbu

Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.
—Yohana 10:16

Nukuu la Ujumbe

"Hakuna aliye na haki ya kusikia injili mara mbili, kama kunasalia yule ambaye hajaisikia mara moja."
—Oswald J. Smith

Somo la Pili
Vikwazo na tofauti za mila

"Na mimi hata sipendi kula samaki!"

Maswali ya Mazungumzo au Kutafakari

Tazama: *Samaki* 00:05:21–00:05:51; *Max na Yusufu wanakutana* 00:13:08–00:18:38

Chakula cha kwanza cha Max pwani ilikuwa kitamu – lakini yeye hakikumpendeza. Kisha anakumbana na tofauti za kidini kwa mara ya anapoishi kwa familia ya Yusufu. Hapo basi katika uzoefu huo, anaelewa hali iliopo ya mapendeleo, na hata vikwazo kati yake, hiyo familia na wengine pwani.

1. Ni tofauti gani za kitamaduni na kidini alikumbana nazo Max wakati akiwa pwani?

2. Tambua maneno, vitendo na/au mitazamo inayoonesha chuki za kidini au tamaduni.

3. Kwa namna gani utamaduni waweza kuwa kikwazo katika mazungumzo? Eleza jinsi ulivyokumbana na kutoelewana na yeyote ambaye ni wa utamaduni tofauti.

4. Yesu na Paulo ni mifano bora ya wahudumu au "wamishonari" katika tamaduni tofauti. Ni hadithi zipi ambazo zinaeleza wakikumbana na utamaduni tafauti nao? Ni vifungu vipi vya maandiko tunasoma kuhusu jinsi ya kushiriki na wale wa utamaduni au dini tofauti nasi?

5. Mambo gani unaweza kufanya "kujenga daraja" na wale wa utamaduni mwingine ili kuweko na uaminifu na sio chuki?



Mawazo ya Mwisho

Injili ya Yesu Kristo ni ya kubadili maisha ambayo ni lazima iwafikie watu wote na makabila yote. Kila kabila, hata hivyo, linayo utamaduni tofauti, hii ni kumaanisha wako na mtazamo fulani wa maisha, na hali tofauti ya kutazama na kufafanua mazingira yao. Wale walio na ujumbe muhimu wa kupeana kwao, mara nyingi hawaelewani vikamilifu wanapozungumza na hapo kupoteza maana kamili ya ujumbe wao.

Ujumbe wetu – Injili – unayo dhamana kubwa kupotelea katika tofauti za utamaduni. Lazima tuhakikishe tunaelewa huo utamaduni mwingine ili ujumbe Wake upokelewe kama ukweli katika utamaduni huo.

Ujumbe wa Aya ya Kumbukumbu

Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao;
—Matendo ya Mitume 17:26

Nukuu la Ujumbe

"Upendo ndio mizizi ya umishenari; kujitolea ndio matunda ya utume."
—Roderick Davis

Somo la Tatu
Mwito

"Na je kuhusu Tume Kubwa? Halisemi tuketi tungojee wanafunzi. Lasema nendeni mkawafanye."

Maswali ya Mazungumzo au Kutafakari

Tazama: *Matukio ya ashera* 00:19:27–00:21:02; *Kumbukumbu* 00:35:45–00:40:58; *Chakula cha jioni kwenye kilabu(mkahawa)* 00:51:58–00:54:04

Kwa kukutana naye Yusufu, max anakabiliwa na ukweli kuhusu waliopotea. Ghafla anaelewa kwamba familia ya Yusufu na jamii yake kwa jumla hawajanufaika na ukweli wa Injili. Max anajibu kwa kuhoji jukumu lake, na kisha hatulii. Tazama jinsi lengo lake linabadilika. Tukio hili moja linamchoma, na kutilia shaka maisha yake ya baadaye.

1. Ni kwa namna gani Max aligundua kwamba familia ya Yusufu hawana habari kuhusu Injili?

2. Ni vipi Max anaonyesha jukumu lake?

3. Mjomba wake Nzomo alimuuliza, "Kwa hivyo umekuwa ukisoma Biblia. Namaanisha, kusoma kikamilifu." Ni vipi kusoma Biblia anaungana na utume? Soma Mwanzo12:1-3, Wagalatia 3:8, na Warumi 10:14-15. Ni vipi vifungu hivi vinahusiana na utume?

4. Kulingana na Maandiko, Ni nani anaitwa kujihusisha na kuwafikia wale hawajafikiwa?

5. Ni vipi utaelewa kama Mungu anakuita ujihusishe kupitia kwa maombi, kutoa mali, ama labda kuenda?

6. Je, kanisa linahitaji kuitwa? Au ni wajibu wa moja kwa moja?



Mawazo ya Mwisho

Ni muhimu kuelewa kwamba Kanisa lote la Kristo linayo jukumu la kuwafikia wale hawajafikiwa. Ukisoma Biblia yako – namaanisha kusoma kikamilifu – unakuwa wazi hivyo. Kwa njia moja au nyingine, sisi kama kanisa lazima tuhusike kuwafikia watu wale hawajafikiwa duniani. Kuitika mwito kutoka kwa Mungu ni muhimu sana. Lazima ushawishike moyoni mwako, kama Max, kwamba ni Mungu aliyekuita. Wakati mtu anapokea mwito, ni lazima kanisa liweze kumkubali na kumtambua ili mishonari atumwe.

Ujumbe wa Aya ya Kumbukumbu

Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao waohubiri habari ya mema!
—Warumi 10: 14-15

Nukuu la Ujumbe

"Wengine hutamani kuishi karibu na watakaposikia sauti za kengele makanisani. Ningependa kuwa na kituo cha kupokea waliopotea nusu mita kutoka ahera."
—C.T. Studd

Somo la Nne
Gharama

"Sio kila mara njia rahisi sio njia sahihi."

Maswali ya Mazungumzo au Kutafakari

Tazama: *Ruth akilia* 00:54:04–00:55:37; *Njia rahisi* 01:16:01–01:17:49; *Chakula cha jioni na Malombe* 1:06:23–01:10:05

Mbeleni, Ruth alionekana kustarehe na maswali Max alikuwa nayo kuhusu jukumu. Lakini wakati Max alipendekeza kurudi pwani na kuanzisha kanisa, alimjibu kwa uoga na kutokuwa na uhakika. Wasiwasi wake ulikuwa halisi. Tajiri wake Max (ambaye ni babake Ruth) alimuonya kwamba atapoteza kila kitu.

1. Ni baadhi ya vitu gani Max ilibidi apoteze ili kufuata mwito wake?

2. Mamake alihofia kupoteza nini?

3. Ruth alihofia kupoteza nini?

4. Mwishowe, mbona kila mmoja wao alikuwa tayari kupoteza kila kitu kwa ajili ya injili?

5. Ni vipi utamshauri Mary (Mamake Max) au Ruth anapokabiliana na mwito wa mtu wampendaye?

6. Ni maneno gani ya faraja utampa mtu sawa na Max ambaye amekumbwa na upinzani dhidi ya mwito wake?

7. Ni kitu gani uko tayari kupoteza ili kufuata mwito wa Mungu ambao ni kuwafanya mataifa yote kuwa wafuasi wake? Na kanisa lako je?



Mawazo ya Mwisho

Yesu alilipa gharama kubwa kwa ajili ya wokovu wa dunia! Ni nani, basi, atalipia Gharama ili kufikisha ujumbe wa wokovu kwa mataifa yote? Ni rahisi. Kanisa la Yesu Kristo lazima liwe tayari kugharamia. Je, kunayo Gharama ambayo ni kuu sana kulipa ili mataifa yote yapate wokovu?

Ujumbe wa Aya ya Kumbukumbu

Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza; naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona.
- Mathayo10:39

Nukuu la Ujumbe

"Sio mjinga yule apeanaye kile hawezi tunza ili kupokea kile asichoweza kupoteza."
—Jim Elliot

"Kama Kristo ni Mungu na alikufa kwa ajili yangu, basi hakuna gharama inayoweza kuwa ghali kwangu kwa ajili yake."
—C.T. Studd

Somo la Tano
Jukumu la Kanisa

"Kwa uaminifu wote, Max, sitajua hata ni wapi pa kuanzia".

Maswali ya Mazungumzo na Kutafakari

Tazama: *Chakula cha jioni kwenye kilabu(mkahawa)* 00:49:48:07–00:51:18; *Mchungaji amfahamisha* 01:42:23–01:43:44; *Ofisini kwa Wambira* 00:42:46–44:34

"Kanisani mwetu hakuna utajiri mkubwa. Na tunayo mahitaji mengi sana kati ya waumini hapa. Kwa hakika, nyingi sana. Wakati mwingine sijui ni nini naweza kufanya. Na pia, kuna wale ambao sio Wakristo hapa kwetu ambao wanahitaji kufikiwa. Kuna mashirika mengine na madhehebu na mataifa ambao wako na uwezo wa kufanya hivyo. Wanazo raslimali."

1. Ni sababu gani Mchungaji Wambira alikuwa nazo kwa nini kanisa lake lisihusike? Je waona hizi kama sababu halali?

2. Kwenye mkahawa, Max, Ruth, Zipporah, na Tom kwa ufupi eleza mtazamo wao kuhusu umishenari? Je waweza kulinganisha tofauti za maoni na mtazamo wa hawa wanne?

3. Hakika, jukumu la kanisa kuwatuma wamishonari ni lipi?

4. Ni vizuizi vipi vilivyoko kushiriki katika utume na kwa namna gani kanisa laweza kuviondoa

5. Kitu gani kanisa lako linafanya kutekeleza jukumu lake la kimishonari? Ni nini zaidi kanisa lako laweza kufanya katika kuhusika kwake na utume?

6. Ni kitu gani haswa waweza kufanya ili kueneza habari za kutuma wamishonari kanisani mwako?

Mawazo ya Mwisho

Kanisa la Antioch lilikubali kuwatuma wawili wao shujaa (Paulo and Barnaba) kwa mataifa. Sisi nasi lazima tuwe tayari kuwatuma shujaa wetu. Lakini, ili hilo lifanyike, lazima tufunze neno – kwa uhalisi – kanisani mwetu.

Lazima waelewe mahitaji ya wale hawajafikiwa. Lazima tuwaongoze kuombea wale hawajafikiwa. Lazima tufunze na kuonesha kupeana kwa ajili ya wale hawajafikiwa. Kama tunao uaminifu kwa haya yote, mwito wa kuenda kwa wale hawajafikiwa utazidi kuongezeka mioyoni mwa watu. Wataanza kuomba, kupeana, na kuenda.

Na wakati kanisa linatumana, lazima liwe tayari kuwatunza wakiwa kazini. Huu ndio msingi wa kanisa kuelewa jukumu lake katika utume, na kazi itendeke vyema.

Ujumbe wa Aya ya Kumbukumbu

Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao —Matendo ya Mitume 13:2-4

Nukuu la Ujumbe

"Alama ya kanisa halisi sio watu walioketi, Lakini uwezo wake wa kutuma wamishonari." —Mike Stachurarun

Somo la Sita
Kujitolea

"Lazima tukamilishe kazi."

Maswali ya Mazungumzo na Kutafakari

Tazama: *Mahubiri (ya)/ kuhubiri kwa Max* 01:44:04–01:55:40

Mungu aliingiza Max katika maisha ya mvuvi, na kwa kufanya hivyo, alibadili mtazamo wa Max kuhusu watu wa utamaduni na imani nyingine. Mungu alimtumia Max kubadili mtazamo wa Mhubiri Wambira, na kuihimiza kanisa kuungana naye katika uamuzi wake wa kuenda.

1. Mambo gani katika hadithi ya Max yanaashiria Kujitolea kwake?

2. Ni shughuli gani Max anajihusisha nazo anapojitayarisha kuenda utume?

3. Mwishowe, Je, Mchungaji Wambira na kanisa kwa jumla walijihusisha na umishenari. In the end, were Pastor Wambira and the church committed to missions? Viashiria vipi waona vya kujitolea kwao?

4. Unafikiri ni nini kitahitajika sio tu kumtunza Max katika utume yeye na familia yake?

5. Ni vipi Mungu ametumia filamu hii kubadili mtazamo wako? Ni kitu gani Mungu anakueleza kufanya? Nini unahitaji kufanya kwanza?



Mawazo ya Mwisho

Takriban nusu ya makundi ya watu duniani wanahesabiwa kama "wamefikiwa" lakini ni nusu iliyo rahisi. Kufikia nusu iliosalia haitakuwa kazi rahisi, na haitafanyika pasipo ya kutia bidii. Itahitaji kujitoea zaidi ya jambo lingine lolote – na hata zaidi ya pesa. Kwa kujitolea kwenda kwa wale hawajafikiwa, na kwa usaidizi wa Mungu, twaweza tukamilishe kazi hii!

Ujumbe wa Aya ya Kumbukumbu

Nalifurahi sana katika Bwana, kwa kuwa sasa mwisho mmehuisha tena fikira zenu kwa ajili yangu, kama vile mlivyokuwa mkinifikiri hali yangu lakini hamkupata nafasi. Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.
—Wafilipi 4:10-13 (soma hadi.18)

Nukuu la Ujumbe

"Ni shughuli jumla kwa kanisa jumla kuhubiri ujumbe jumla kwa dunia nzima." —Charles H. Spurgeon

Na wewe Je,?

Andika mpango wako jinsi utakavyojihusisha na shughuli za utume katika kanisa lako. Kila mmoja wa kikundi cheni anaweza kutambua ni lipi jukumu lake katika shughuli za umishenari. Waweza kuwa mtu wa kutafuta watu au raslimali, wa kuomba, wa kuihimiza, mishonari, kupeana pesa, na kadhalika.

Fikiria kuhusu hilo. Omba kwa ajili ya hilo.

Kikundi kichotayarisha masomo kuhusu Mashua Ya Mbali:

Rev. Gilber Jumba
(mwenyekiti)

Wairimu Kamau

Rev. Anthony Bones

Phil Harman

Starlene Harman

Lucy Kega

Luch Wachira

Edward Olukune

Dan Germo

Kwa habari zaidi tembelea http://fttafriserve.org
www.distantboat.com

Vipengele vimetolewa kwenye Bibilia Takatifu toleo la Kiingereza (ESV®), hati miliki © 2001 ya Crossway, chapisho la Good News Publishers. Zimetumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa